

Tangazo la redio imetolewa na Traffic Police Radio Uhuru FM
Mei / Juni 2010

Maegesho/Parking

Ahsante sana Ndugu mtangazaji, kwanza kabisa ningependa wasikilizaji na wananchi wote kwa ujumla wanaosikiliza Radio Uhuru FM kwa sasa wafahamu kuwa maegesho yote ya magari ypo hapo yalipo kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 na kama ilivyofan nywa marekebisho ya mwaka 2002 kifungu 1 & 72. Kifungu cha 71 cha sheria hiyo ya usalama barabarani kinampa waziri husika mamlaka ya kutenga eneo la pembeni mwa barabara kwa ajili ya maegesho na magari ya aina tofauti anavyoona inafaa.

Na kifungu cha 72 cha sheria hiyo hiyo kinae elezea bayana kabisa mamlaka aliyonayo waziri kutenga maeneo kwa ajili ya maegesho maalum kwa ajili ya mabasi, taxicab na maeneo maalum kwa ajili ya kubebea na kushushia mizigo. Tunapoong gelea maegesho maalum ndugu mtanganzaji na wasikilizaji wanaonisikiliza hivi sasa ingependa wafahamu kuwa ni makosa kwa gari ambalo halip kwenye kundi hilo la kuegeshwa kwenye eneo hilo kwa mda mrefu unaozidi tuseme dakika tano. Kwa mfano, wenye vituo vya mabasi kukuta taxi, nalori au gari za binafsi zimeegeshwa.

Ndugu mtangazaji maegesho yapo aw yametengenezwa kwa ajili ya kuhifadhi magari kwa muda mrefu au muda mfupi kuwawezesha wenye magari mbalibali kufanya shughuli zao na wakati huo huo kutowazuia watumiaji wengine wa barabara kuendelea kutumia barabara, kwa hiyo ni makosa na unastahili kuchukuliwa hatua za kisheria endapo utakutwa umeegesha gari au kupakia na kushusha mizigo kwenye njia ya waendao kwa miguu. Mfano Uhuru Rd. maeneo ya kwanzia shule ya Uhuru mpaka clocktower mnara wa saa.

Maegesho kwa kawaida yako ya aina tatu na mara nyingi huwa kuna msaada wa michoro ya mistari ikionyesha ni jinsi gari unatakiwa kuegesha gari yako kuna kuegesha gari kwa WIMA, MSHAZALI (Inclined) na ya MSTALI.

Unapotaka kuegesha gari yako au kusimama ni lazima kwa dereva aliyefuzu vizuri mafunzo yake ya udereva kuangalia kwanza vioo vyake yaani side mirrors au driving mirror, kisha kutoa Ishara kwa watumiaji wengine wa barabara na kisha ndipo sasa unaweza kufanya kitendo cha kusimama au kuegesha. Tunawashauri madereva kutoka nje kabisa ya barabara wanapokwenda kwenye maeneo yanayofaa kwa kuegesha. Na Iwapo kuna dharura yeyote ya kukulazimisha usimame barabarani, basi simama kadri iwezekanavyo uapnde wa kushoto ili kuweza kuruhusu matumizi ya barabara kwa wengine. DAIMA angalia eneo unaloegesha gari yako ni salama na inaruhusiwa kisheria usiegeshe eneo lililo katazwa.

Kabla ya wewe dereva au abiria wako kufungua mlango, hakikisha hutamgonga mtu yeyote anayepita barabarani au kwenye njia ya watembea kwa miguu, waendesha baiskeli pikipiki. Ndio maana tunawataka wanaoshuka kwenye magari watumie upande wa kushoto karibu na ukingo wa barabara.

Mabo ya Msingi ndugu mtangazaji na wasikilizaji wanaeosikiliza Radio Uhuru FM ambayo inabidi wayafahamu kabla ya kuegesho magari hayo.

1. Kuwajali na kuwafikiria watumiaji wengine wa barabara.
2. Kwenye Alama za pundamilia au mia 5 karibu na Alama hizo.

3. Mita 5 ndani ya makutano ya barabara au mahali reli inapokatisha barabara.
4. Kwenye kituo cha basi au mita 15 toka pande zote za alama ya kituo cha Mabasi.
5. Kwenye njia ya watembeao kwa miguu.
6. Mbele ya sehemu ya kwingilia magari.
7. Barabara yenye mistari myeupe miwili ya katikati hata kama moja ya mistari hiyo imekatikakatika.
8. Usipaki pasipo alama ya parking au mistari ya njano kwenye kingo za barabara.

Usiegeshe mahali popote ambapo itakuwa hatari au kusababisha matatizo kwa watumiaji wengine wa barabara kwa mfano:

1. Kalibu na geti la shule
2. Karibu na kilele cha kilima
3. Kwenye kona kali
4. Upande mwingine wa gari lililo egeshwa (uegeshaji wa magari mawili)
5. Pale ambapo gari lako litakiziba kituo cha taxi
6. Pale gari lako litaziba alama au ishala za barabarani

Hakikisha unapoliacha gari lako baada ya kuegesha kamwe usiliache gari bila kuzima ingini, taa na hakikisha pia breki ya mkono nayo imewekwa. Funga gari lako daima. Uegeshaji wa magari kwenye barabara zenye magari mengi na yanakwenda kwa kasi hautakiwi iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo basi washa taa za kuegeshea (parking light) na egesha gari lako upande wa kushoto wa barabara tu.